

TANGAZO LA SERIKALI Na. 51 la Tarehe 24/1/2025

**KANUNI ZA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA  
(TS. Na. 368 la 2009)**

**AMRI**

*(Imetolewa chini ya Kanuni ya 6(2))*

AMRI YA MAREKEBISHO YA AMRI YA KUENZISHA MASJALA NDOGO ZA  
MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA YA MWAKA 2025

Jina na kuanza  
kutumika  
TS. Na.  
368 la 2009

**1.-(1)** Amri hii itajulikana kama Amri ya Marekebisho ya Amri ya Kuanzisha Masjala Ndogo za Mahakama ya Rufani ya Tanzania ya Mwaka 2025 na itasomwa pamoja na Amri ya Kuanzisha Masjala Ndogo za Mahakama ya Rufani ya Tanzania ya Mwaka 2022 ambayo hapa itarejewa kama “Amri kuu”.

(2) Amri hii itaanza kutumika tarehe 31 Januari 2025.

Marekebisho ya  
Jedwali

**2.** Amri kuu inarekebishwa katika Jedwali kwa kuongeza neno “Dar es Salaam” kwa kufuata mpangilio wa kialfabeti.

Dar es Salaam,  
21 Januari, 2025

IBRAHIM HAMIS JUMA,  
*Jaji Mkuu*